

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

ISO 9001:2015 CERTIFIED



**TAARIFA KWA UMMA**

**WITO WA KUSHIRIKI KATIKA TUZO ZA “SDG DIGITAL GAMECHANGERS” KWA MWAKA 2024**

Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (ITU) pamoja na wadau wake wanawaalika wadau wote, kutoka serikalini, sekta binafsi, vyuo vikuu, asasi za kiraia, jumuiya ya wataalamu wa TEHAMA, na vijana kushiriki katika toleo la pili la Tuzo la SDG Digital GameChangers - kutambuliwa kwa kimataifa kwa miradi mipya, programu na sera zinazotumia teknolojia ya kidijitali kufikia Malengo 17 ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs).

Washiriki wanaalikwa kushiriki katika kipengele mojawapo ya (Watu, Sayari, Ustawi, Amani) kila moja ikiwa sambamba na lengo lake la SDGs mahususi. Vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 29 pia wanaweza kushindania Tuzo ya Vijana Waasisi Mahiri kwa kuwasilisha ubunifu zao na miradi ya kidijiti ambayo inachochea mabadiliko makubwa duniani kote.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Tuzo la SDG Digital GameChangers, ikiwa ni pamoja na fomu ya kuwasilisha mtandaoni, masharti na vigezo, mchakato wa kuchagua washindi, na masharti mengine tafadhali bofya viunganishi hivi <https://www.itu.int/initiatives/sdgdigital2024/award/submission-form/> na <https://www.itu.int/initiatives/sdgdigital2024/award/terms-and-conditions/>.

Kwa kushiriki katika Tuzo la SDG Digital GameChangers, utakuwa na fursa ya kutambuliwa kwa kazi yako yenye matokeo chanya katika jamii, kushirikiana na watu wenye nia moja, na kuwa mshiriki katika tukio la kimataifa linalolenga katika matumizi ya taarifa (data) na TEHAMA kwa ajili ya maendeleo endelevu. Washindi Watano (5), mmoja kwa kila kipengele, watatunukiwa tuzo tarehe 20 Septemba 2024, New York, Marekani.

Ukomo wa mawasilisho yote ni tarehe 11 Agosti, 2024 saa 6:00 usiku, Saa ya Afrika Mashariki.

Imetolewa Tarehe **11 Julai 2024**.

Dkt. Jabiri K. Bakari  
MKURUGENZI MKUU

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.

Simu: +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Nukushi: +255 22 2412009-10

Barua pepe: barua@tera.go.tz, dg@tera.go.tz, Tovuti: www.tera.go.tz